



**4th COMMUNITY OF PRACTICE FOR LEARNER-CENTRED
EDUCATION**

Dec 2011 CONFERENCE

KUIMARISHA UPIMAJI ILI KUKUZA UJUZI

Imetayarishwa na:

Joyce Andrew- Mkaguzi wa Shule Manispaa

SHINYANGA

KUIMARISHA UPIMAJI ILI KUKUZA UJUZI

UTANGULIZI:

Elimu inalenga zaidi katika kupata suluhu ya matatizo ambayo yanatukumba lakini wakati mwingine hatujui chanzo chake. Hivi sasa ufundishaji unaozingatia kujenge ujuzi umeanza kutumika badala ya ule wa zamani ulikuwa unamuona mwalimu kama kiini pekee cha ujifunzaji. Ufundishaji unaozingatia ujuzi unatakiwa kumfanya mwanafunzi kuwa mbunifu katika tendo la kujifunza na kuyatumia yale aliyo jifunza. Mtazamo huu unamfanya mwanafunzi aweze kujenga maana ya kile anachojifunza na hivyo kufanya tendo la ufundishaji na ujifunzaji kuwa rahisi zaidi na lenye kumvutia mwanafunzi. Na pia kumfanya Mwalimu kuwa mwongozaji na mchokozaji wa mada badala ya kuwa ghala pekee la maarifa. Ufundishaji unaozingatia ujuzi unalenga katika kumpatia mwanafunzi maarifa, ujuzi na stadi zitakazomwezesha kujifunza kwa kujitegemea zaidi pamoja na kukabili maisha yake baada ya kumaliza shule.

Hata hivyo ili ujuzi na stadi ziweze hizo kujengwa hatuna budi kuhakikisha kuwa ufundishaji unakuwa sio ule ambao ni wa kumkaririsha mwanafunzi na badala yake uwe wenye kumjengea uwezo wa kiutendaji zaidi.

Mbinu na njia za kufundishia na kujifunzia ziendane na mabadiliko ya mtaala ambao ni shirikishi zinazolenga kumjengea mwanafunzi uwezo wa kufikiri na kutenda. Lengo ni kumwezesha kuwa na mwelekeo chanya katika maisha yake. Aweze kutafakari katika kila hatua ya utendaji na baadaye atafakari pia kuhusu mwendelezo wa stadi aliyojengwa.

UPIMAJI:

Upimaji unahusu maudhui. Mwanafunzi anaelewa nini? Anajifunza nini?. Kwa upande mwingine upimaji ni mchakato. Namna gani mwanafunzi anajifunzi. Jinsi anavyoibua maarifa na kuyaendeleza. Hivyo upimaji unahusu uhusiano uliopo kati ya mwalimu na mwanafunzi katika mchakato wa kujifunza. Je wanafunzi wanatumia wanatumia mbinu za kufikiri kwa kina?

Je wanaweza kueleza na kutatua matatizo? Wanatoa mawazo kwa usahihi? Je wanahusishaje imani walizonazo na uzoefu katika kujifunza. Haya ndiyo maswali ya kujiuliza katika mchakato wa upimaji, pamoja na njia ambazo maarifa yanatolewa ndani ya darasa.

UPIMAJI KATIKA ELIMU:

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi imetoa sera na miongozo kadhaa inayosimamia upimaji katika elimu. Zipo njia/mbinu nyingi ambazo wakati wa mafunzo ya ualimu zinaelekezwa kuzitumi katika kuwapima wanafunzi. Lakini njia ambazo zimekuwa zikitumika zaidi katika shule na ndani ya darasa ni maswali na majibu, mazoezi wakati wa kufundisha na mwisho wa mada, mitihani/majaribio ya wiki au mwezi na mitihani mikubwa ya kumaliza mihula, mwaka na shule. Katika njia/ mbinu hizo mitihani imepewa nafasi kubwa zaidi katika upimaji, na hivyo hata mtazamo wa ufundishaji shuleni umefikia hatua ya kuathirika, kuyumba na kuwa na mtazamo zaidi wa maandalizi ya kufaulu mitihani tu.

Pamoja na kuwa mtaala umeboreshwa na mtazamo umebadilika na kulenga kukuza ujuzi kwa mwanafunzi lakini upimaji unaendelea kuwa wa kutegemea mitihani kuwa ndio kipimo cha uelewa wa mwanafunzi

Hali hii kama ambavyo imekuwa ikizungumzwa mara kwa mara, imefikia hapa kutokana na;

1. Walimu wengi kuwa na uwezo mdogo wa kutawala mada za masomo yao hasa hisabati, English na sayansi, vivyo hivyo uwezo wao wa kupima maendeleo ya wanafunzi, unakuwa duni. Hivi sasa Walimu wengi wanatoa mitihani isiyoendana na mfumo wa utungaji. Wengi wao wamejikita katika kukaririsha mitihani ya nyuma.
2. Kukosekana kwa usimamizi na ufuatiliaji madhubuti wa kazi za walimu shuleni, hali hii inasabaisha walimu wengi kutokamilisha mihutasari au kutofundisha kabisa baadhi ya mada za masomo na kutowapima ipasavyo wanafunzi. Hali hii inakuwa mbaya zaidi kutokana na kuwa Walimu wakuu na walimu wa Taaluma ambao hawakupatiwa mafunzo yoyote hata baada ya kupewa nyadhifa hizo.

3. Shule kutokaguliwa kwa muda mrefu hali inayotokana na Idara ya Ukaguzi wa shule kutokupewa mafungu ya kazi kwa muda mrefu. Hali hii imefanya walimu kutojali kazi na hasa wanapokuwa na madai yasiotimizwa kwa upande mmoja na kubanwa na jamii kwa upande mwingine.
4. Utoro wa wanafunzi, hali hii inaweza kutokana na ukosefu wa chakula cha mchana shuleni, wanafunzi hushinda na njaa na hivyo kushindwa kufuatilia masomo ipasavyo. Pia kwa shule nyingi nje ya miji zipo katika mazingira yasio na maji wala vyoo vya kutosha

NINI KIFANYIKE/MAPENDEKEZO:

Ili kuweza kufikia malengo ya mtaala na kunfanya mwanafunzi kupata ujuzi uliokusudiwa tunahitaji kuwa na utaratibu mpya na thabidi katika upimaji.

Madhumuni ya upimaji kama yalivyo na yakifuatwa inavyotakiwa ni mazuri kabisa lakini tunahitaji kufaya yafuatayo:

1. Pawepo na ushirikiano wa Taasisi/vyombo vinavyosimamia masuala ya elimu mfano TIE, NECTA/UKAGUZI WA SHULE na Mafunzo ya ualimu.
2. Vigezo vya kufaulu
Ipo haya ya kuvitazama upya vigezo vya ufaulu vinavyotumika kwa sasa. Mtahiniwa asihesabiwe kuwa amefaulu kwa kutumia matokeo ya mtihani peke yake. Matokeo ya mtihani wa mwisho yachukue 50%. Sehemu iliyobaki igawanywe kwa mazoezi ya darasani, kazi za mikono na kazi miradi (project) ambazo mwanafunzi atahitaji kukusanya taarifa na kuzifanyia uchambuzi
3. Utungaji wa mitihani ya kumaliza shule
Utungaji wa mtihani ya kumaliza shule unatakiwa uendane na mtaala unaozingatia ujuzi ili kumwezesha mwanafunzi kupata ujuzi uliokusudiwa na uweze kumsaidia katika kukabiliana na changamoto mbalimbali zinazojitokeza katika maisha yake ya kila siku.
4. Mambo ya msingi katika kukuza ujuzi wa mwanafunzi

Ili kukuza ujuzi wa mwanafunzi na kupata zao tokeo katika ufundishaji na ujifunzaji wa mwanafunzi kuna mambo yanatakiwa kufanyika

- Mawasiliano

Mwanafunzi anatakiwa kuwa na uwezo wa kujieleza kutoa mawazo yake na mtazamo wake kuhusiana na jambo analojifunza. Kutoa na kupokea taarifa kwa umakini ili kumwezesha kukuza uwezo wake wa kuwasiliana na wenzake kwa mazungumzo na kwa maandishi ikiweko kuwa na ujuzi wa kuzungumza na kuandika lugha ya kufundishia kwa kuwa lugha ndicho kiini cha ujifunzaji katika masomo yote.

- Hesabu

Mwanafunzi anatakiwa awe na ujuzi wa msingi wa hisabati ili kumwezesha kujifunza fani mbalimbali.

- Ubunifu na kufikiri kwa kina

Mchakato huu wa kufikiri kwa kina utamsaidia mwanafunzi kuwa na uwezo wa kupata maarifa, ujuzi, stadi na mwelekeo yatakayomwezesha kutumia ujuzi kwa manufaa yake na kwa maendeleo ya jamii. Ataweza kufanya maamuzi sahihi na kwa wakati.

- Teknolojia

Ujuzi huu utamsaidia mwanafunzi kutambua umuhimu wa teknolojia kwa jamii na kukuza maarifa kuhusu teknolojia zilizopo, njia za kuzitumia na hivyo kumfanya ajimini, kubuni na kutumia teknolojia katika kutatua matatizo ya jamii.

- Stadi za mahusiano (Interpersonal Competences)

Uwezo wa mwanafunzi kupima mawazo ya wengine. Pia kushiriki na wenzake katika makundi ya ujifunzaji.

- Uwezo wa mwanafunzi kujifunza peke yake

Mwanafunzi kuwa na uwezo wa kujifunza kwa kujitegemea pasipo kumtegemea mwalimu, kuwa na motisha ya ndani inayomwezesha kujifunza kila siku ili kukuza

stadi za maarifa, ujuzi na mwelekeo na kupata maarifa kutoka katika vyanzo mbalimbali

5. UPIMAJI DARASANI

Ili kukuza na kuendeleza upimaji darasani hatuna budi kuwa na mwongozo juu ya upimaji darasani ili kuhakikisha kuwa upimaji unalenga kupata picha ya maendeleo ya kukua kwa uelewa, kujifunza kwa kina na Nyanja za juu za kufikiri za maarifa stadi na mwelekeo.

Njia za upimaji zitumike kama ifuatavyo:-

- Mahudhurio 5%
- Mazoezi darasani 5%
- Kazi za mikono ndani na nje ya darasa 5%
- Mitihani ya mwezi 5%
- Mitihani ya mihula 10%
- Mitihani ya mwaka 20%
- Mitihani ya Taifa 50%

Kwa kutumia zana za ufuatiliaji wa mwanafunzi mmojammoja kwa somo, mwalimu atatakiwa kutunza kumbukumbu juu ya yote aliyoyafanya juu ya yote aliyoyafanya na matokeo yake.

6. UFUATILIAJI WA UPIMAJI

Katika kuimarisha na kuboresha upimaji wa wanafunzi, inatakiwa pawepo ufuatiliaji endelevu wa upimaji katika ngazi mbalimbali.

Mara moja kwa mwezi walimu wote watafanya kikao cha ufuatiliaji kuona mwenendo wa upimaji na mambo yanayojitokeza.

Walimu wakuu wawe na jukumu la kusimamia ufundishaji unaoendana na maboresho ya mtaala ya mwaka 2004 na upimaji wake.

Waratibu elimu kata wanatakiwa kujipanga ndani ya miezi miwili watashiriki angalau mara moja katika vikao vya shule zilizo kwenye kata zao. Pia kila robo mwaka kutoa taarifa ya hali ya upimaji na ufundishaji katika shule za kata zao kwa Afisa Elimu.

Maafisa Elimu wagawane maeneo ya shule ya kufuatilia na washiriki katika vikao vya elimu vya kata na vya walimu. Suala la upimaji liwe linatolewa taarifa za ufuatiliaji kwa madhumuni ya kuimarisha ufundishaji unazongatia ujuzi.

Wakaguzi wa shule wafanye ufuatiliaji wa upimaji wa darasani ili kufanya thatmini na kuhakikisha kuwa upimaji ni sahihi kwa mujibu wa taratibu za ufundishaji wa mtaala unaolenga zaidi mwanafunzi.

Reference

1. Primary School Leaving Examinations; School-level efforts to improve Performance

Septini Kitta, Rebecca Sima and Suleima Sumra(March 2008).

2. Redefining Quality Education in Tanzania; From inputs to capabilities

HakiElimu (October 2007)

3. Primary School Leaving Examinations; What do the examinations measure ?

Septini Kitta, Rebecca Sima and Suleima Sumra(March 2008).

4. Primary School Leaving Examinations; A study on the increases in pass rates

Suleima Sumra (March 2008).

- 5 East African Education Publishers (Ltd) Primary Education ***Joseph Ngaroga***

- 6 Institute of Continuing Education Diploma in Primary Teachers Education (November 2008) General Teaching Methods and strategies ***Cornellia Muganda Et ...Al***